# MSIYASAHAU MATENDO YA MUNGU

Lauriano Nyoni
September, 2025
Dodoma

**Wimbo wa katikati**
**Kutukuka kwa Msalaba**




1. Enyi watu wangu sikilizeni sheria yangu/
   tegeni sikio kwa maneno ya kinywa changu/
   nifungue kinywa changu kwa mithali/
   niyatamke mafumbo ya kale.
2. Alipouawa ndipo walipoanza kumtafuta/
   wakarudi wakamtaka Mungu kwa bidii/
   wakakumbuka kuwa Mungu ni mwamba wao/
   na Mungu aliye juu ni mkombozi wao.
3. Lakini walimdanganya kwa vinywa vyao/
   wakamwambia uongo kwa ndimi zao/
   kwa maana mioyo yao haikuwa thabiti kwake/
   wala hawakuwa waaminifu katika agano lake.
4. Lakini yeye kwa kuwa ana rehema/
   husamehe uovu wala haangamizi/
   mara nyingi huipitisha mbali ghadhabu wake/
   wala haiwashi hasira yake yote.